



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA KIBITI



Kibiti.

12 Aprili, 2023.

## TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti Ndg. **Mohamed I. Mavura**, anapenda kuutaarifu umma kuwa kwa kipindi cha **Julai 2022** hadi kufikia **Machi 2023** Halmashauri imepokea kutoka Serikali kuu kiasi cha shilingi **1,944,831,178.06** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Fedha hizi ni sawa na asilimia 76.56 ya lengo la Mwaka 2022/2023. Ifuatayo ni Miradi itakayotekelezwa kwa fedha hizi:-

1. Kiasi cha shilingi **424,478,978.06** kwa ajili ya ukamilishaji wa Jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.
2. Kiasi cha shilingi **150,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.
3. Kiasi cha shilingi **66,103,000.00** Fedha za mfuko wa Jimbo kwa ajili ya Miradi iliyoibuliwa na jamii katika Kata zote za Wilaya ya Kibiti.
4. Kiasi cha shilingi **100,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Zahanati 68 zilizopo Wilayani Kibiti.
5. Kiasi cha shilingi **100,000,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati katika Vijiji vya Nyakaumbanga na Nyambwanda.
6. Kiasi cha shilingi **150,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwa vituo vitano vya afya.
7. Kiasi cha shilingi **100,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya afya ya kinywa na macho katika Hospitali ya Wilaya.
8. Kiasi cha shilingi **88,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo Vituo Shikizi vya Mweyubaruti, Nyambele, Beta, Usimbe, Ndungutu, Zimbwini, Nyambangala na Kimbendu.
9. Kiasi cha shilingi **180,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa Shule kongwe za Msingi za Mchinga, Mfisini, Nyambili, Kiasi, Kiongoroni, Mjawa, Kimbunga na Nyakinyo.

10. Kiasi cha shilingi **156,250,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa Shule za Msingi za Bungu, Tomoni, Mangombela, Jaja, Mahege, Ngalengwa, Kiasi, Msala, Kikale na Mfisini.
11. Kiasi cha shilingi **90,000,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji ujenzi wa maabara katika Shule za Sekondari za Ruaruke, Mjawa na Zimbwini.
12. Kiasi cha shilingi **50,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa bwalo Shule ya Sekondari Mahege.
13. Kiasi cha shilingi **50,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa uzio na ukamilishaji wa bwani la watoto wenye mahitaji maalum Shule ya Msingi Kitundu.
14. Kiasi cha shilingi **60,000,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa mabweni Shule za Sekondari Ruaruke na Zimbwini.
15. Kiasi cha shilingi **200,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika Shule za Msingi za Jaja, Maparoni, Makima na Mkenda

Vilevile, Halmashauri imepokea kiasi cha shilingi **1,339,871,389.02** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ya Elimu ikiwa ni pamoja na Elimu bila malipo Shule za Msingi na Sekondari.

Hivyo, Wananchi wote, viongozi wa ngazi za Vitongoji, Vijiji na Kata mnaombwa kushirikiana ipasavyo katika kuhakikisha kuwa Miradi yote inakamilika kwa wakati sahihi na kwa ubora wa hali ya juu.

Aidha, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti anatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya maendeleo Wilayani Kibiti, hali ambayo inazidi kuipa heshima kubwa Wilaya ya Kibiti pamoja na kuboresha hadhi ya miundombinu ya Elimu, Afya, Barabara, Maji na Umeme.



Cecilia B. Dembe

**Kaimu Mkuu Wa Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini  
HALMASHAURI YA WILAYA KIBITI**